

Taarifa ya Tanga City Council Workshop

Imeandikwa na Dominata Rwechungura

Tarehe 27.5.2009 nilikutana na Jumanne yeye ni mgonjwa alinipa rafiki yake kunitebeza barabarazote za manispaa ya Tanga nilikodi baisikeli mbili kila moja Tsh 2,500 sawa na Tsh 5,000 toka asubuhi mpaka jioni ukweli barabarazote za Tanga hakuna barabara ya wapanda baisikeli walemavu wala maguta, na kwenye Ramani nimeonyesha sehemu ambapo wapanda baisikeli hugongwa sana. Ziara ya tarehe 27.5.2009 ilinisaidia sana kwenye workshop ya tarehe 28.5.2009 niliweza kuchangia vizuri sababu barabara zote nilishaziona.

Siku ya workshop tarehe 28.5.2009 tulifanya ziara ya kutembelea nyuma za kare zilizojengwa na wajerumani pamoja na barabara kama ratiba inavyoonyesha. Upane wa bicycle traffic UWABA tulifanya vizuri pia sababu tulikukuwa tunafahamu sheria za barabara tulitoa ushauri kwa kuwa Tanga wapanda baisikeli ni wengi kuliko magari ni vyema wakipanga miundombinu waweke barabara ya baisikeli.

Madiwani na Meya walikubali na wanapanga namna ya kutupa mwaliko UWABA kutoa elimu kwa wapanda baisikeli.

Baada ya ziara tulijifunza kwa makundi kundi letu lilifanya vizuri pia.

Tulitangaza UWABA Mejah alifanya kazi nzuri sana pamoja na Dominata nilinunua Reflecta jaketi 1 pamoja na helmet 1 kwa ajili ya kutoa zawadi kwa Meya wa Jiji la Tanga ili kuwamasisha wapanda baisikeli kujua sheria za barabarani. Zawadi hizo zilijenga jina la UWABA pamoja na mashirika mengine yalifuarhishwa na mchango wa UWABA kwenye jamii na walisema kutualika ili kutoa elimu ya sheria za barabara.

Mapendekezo

Tanga walipendekeza kufungua ofisi ya UWABA

Watembea kwa miguu nao wanahitaji kujufunza sheria za barabarani.